# WEWE U NANI

*2Timotheo 1:9 – 10*

*Ambaye alituokoa akatuita kwa mwito mtakatifu, si kwa kadiri ya matendo yetu sisi; bali kwa kadiri ya makusudi yake Yeye na neema yake. Neema hiyo tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele.*

Sikiliza Nabii wa Mungu alivyosema juu ya hilo:
Kama utaweza tu kuondoa hali ya hofu/woga katika Kanisa na uwaache wajitambue wao ni nani na wanayo nafasi gani, uponyaji utakuwa ni ujumbe rahisi sana kuhubiriwa au kitu kingine chochote. Lakini mna woga. Mnaogopa, hamtambui kwamba ni wana na binti wa Mungu. Na sasa, sio tutakuwa, bali sasa hivi tu wana na binti za Mungu. (Wagalatia 4:6). Siyo jambo la mbeleni siku zijazo. Na sio wakati ujao huko mbeleni tutaketi katika ulimwengu wa Roho, sasa hivi tumeketi katika ulimwengu wa Roho, sasa hivi (Waefeso 2:6). Na sasa tu wana na binti za Mungu. Bado haijadhihirika tutakuwaje pale mwishoni, lakini tunajua tutamuona Yeye, kwa maana tutakuwa na mwili kama wa kwake (1Yoh. 3:2 – 3 ).
Tunamuona Yeye kama alivyo. [ 1 ]

Na ninashangaa juu ya hilo, kama tutaenda pale nyuma pale mwanzoni, vitu vyote vinaanza pale mwanzoni. Na tunaona pale mwanzo, Mungu alimuumba mtu kwa ajili ya ushirika. Mungu alipenda kushuka chini na kuwa na ushirika na watu wake. Mungu, Pale Mwanzo …… Mwanzo 1: Pale Mwanzo, Mungu ……..” Lile neno pale katika Waebrania ni “El – Elah – Elohim, Yule aliye wakujitosheleza; yule aishiye mwenyewe; mwenye nguvu”. Na ndani yake kuna sifa ya kuwa Baba; ndani Yake sifa ya kuwa mwana, ndani yake kuna sifa ya kuwa mwokozi; ndani yake kuna sifa ya kuwa mponyaji; ndani yake kuna sifa ya Mungu. Hakuna chochote ila Mungu na Mungu pekee.

Sasa, hizi sifa zilizokuwa ndani yake zilifanya vitu fulani vijitokeze ili kumwabudu. Kitu cha kwanza alifanya ni viumbe wa kimalaika, nao wakamwabudu yeye; hawangeweza kuanguka. Ndipo akamweka katika mwili; akaanguka kwa utashi wake mwenyewe, akiwa amepewa uhuru wa kuchagua jema na baya.

Lakini Mungu, pale mwanzo (nakisia, nafikiri) ilikuwa ni wakati wa utukufu sana, wakati Mungu wetu wa thamani na wa Neema aliposhuka katika bustani ya Edeni wakati wa utulivu naye akawa anazungumza na Adamu na Hawa, na wangekuwa na ushirika (Mwanzo 2:15 – 17) [ 2 ]



Walikuwa watoto wake wapendwa. Na waliwekwa katika msingi wa uhuru wa uchaguzi (1Tim 2:3 – 4 ).

Yule asiyeamini Mungu mara nyingi alisema, “Kwa nini Mungu mwenye haki afanye jambo kama hilo. “vema sasa, kama Mungu ni mwenye uwezo wote, kwa nini aliyaachilia haya hata yatokee? Kwa nini hakumfanya mtu kuwa mkamilifu?

Kwa sababu pale mwanzo hakukuwa na kitu ila Mungu. Na ndani ya Mungu kulikuwa na sifa, sifa zake kuwa mwokozi. Tunajua ni hivyo. Yeye ni mwokozi, na hiyo ilikuwa ndani yake. Na hakukuwa na kilichopotea ili kiokolewe. Ndani Yake kulikuwa na sifa ya kuwa Baba, na hakuna cha kulea kama Baba, ndani Yake kulikuwa na sifa ya kuwa mponyaji. Hakukuwa na kilichopotea, wala mgonjwa. Kwa hiyo jambo pekee aliloweza kulifanya ni kuumba mtu katika hali ya uhuru wa kuchagua, akijua kuwa atakosea. Mungu hakulifanya mwenyewe, Mtu ndiye mwenyewe aliyelifanya.

Nawe uko hivyo hivyo asubuhi hii ya leo. Unaweza ukakubali uzima au uukatae. Lakini Mungu amemuumba mtu hivyo, kwamba ange ……. Akijua kuwa atalifanya hilo. Siyo mapenzi yake alifanye hilo, lakini akijua mtu angelifanya hilo, kwamba ingedhihirisha sifa zake. Kwa hiyo hakuna ambacho kiko nje ya muda. Kila kitu kinaenda sawa kabisa na utaratibu mkuu wa muda wa Mungu. Unaona? Na hilo linadhihirisha sifa zake, kuchagua hasa watoto wake ambao wanampenda Yeye hasa na kumuamini. Na kila mtu anayo haki sawa. [ 3 ]

Sasa, kumbuka, unasema, vema, tunaamini hili lakini hatuamini lile” Kama umeolewa na Kristo, Kristo ni neno la Mungu. Mtakatifu Yohana 1 alisema, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, na Neno alikuwa Mungu. Na Neno alikuwa Mungu” Na Neno alifanyika mwili na akakaa nasi. Kristo alikuwa Neno lililohai. Siku zote alikuwa Neno; na bado yeye ni Neno, na siku zote atakuwa neno.

Yeye alikuwa tu udhihirisho wa sifa za Mungu, kwa maana alikuwa mwana wa mungu (Mithali 8:22 – 31), na kila mwana ni sifa za baba yake. Na kama vile tu ulivyokuwa ndani ya chembe ndogo za baba yako, katika mwili wa baba yako alipokuwa kijana mdogo……. Ulikuwa ndani yake, na bado asingeweza kuwa na ushirika nawe. Kwa sababu hakukujua wewe. Lakini kupitia kwa mahusiano na mama, ulilетwa duniani na ukawa katika sura ya Baba; hapo sasa aliweza kuwa na ushirika nawe. Na kadhalika mlikuwa wana wa Mungu na binti za Mungu kabla haujakuwepo hata mwezi, nyota au chochote (Ayubu 38:4 – 7); mlikuwa wana na binti za Mungu. Kwa maana wewe ni udhihirisho tu wa sifa zinazoonekana zilikuwa ndani ya Mungu pale mwanzoni. Kwa maana upo uzima wa milele wa aina moja tu, na huo ni wewe kabla ……..hujui chochote juu ya hilo; pia hukujua ya kuwa ulikuwa ndani ya baba yako wa dunia. Lakini ulidhihirishwa katika sura yake.

Umeumbwa katika sura ya Mungu (Mwanzo 1;27) na ulidhihirishwa utukufuni ukawa na ushirika na Mungu (Efeso 1:3 – 6). Na kwa hiyo, kama kwa hakika

chembe zako ndogo za uhai zilikuwa ndani ya baba yako kabla ya kuzaliwa kwako kimaumbile, chembe ndogo za uhai wa kiroho zilipaswa ziwe ndani ya Mungu, kwa sababu wewe ni udhihirisho wa sifa za mawazo yake kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, hiyo ni kweli. Hakuna njia ya kuzunguuka hilo, hiyo ni kweli. [ 4 ]

Mwanzoni mwa uumbaji wa mungu wakati Mungu alipoanza kuumba na kukuleta wewe uwe aishiye …….. unaona, ulianza pale kama mbegu na ukaendelea kufikia ulipo sasa. Na tena mlikuwa nyote ndani ya Kristo. Hapo Kristo alipokuja, alikufa awakomboe ninyi wote, nawe u sehemu ya hilo neno. Na yawezekanaje Biblia….. yote ni kanuni juu ya kanuni mstari juu ya mstari, hapa kidogo na hapa kidogo, hakuna hata yodi moja au nukta itakayoshindwa …… Itawezekanaje wewe katika dunia, ukiwa ni sehemu ya Neno, ukakatae yoyote ya hilo au nyingineyo yote au sehemu yake?

Kama Roho Mtakatifu ndani yako anakufanya unene kwa lugha, angali nyuma pale na hukubaliani na nyingine yeyote ya Neno, hapo sasa ni roho isiyo sahihi. Unaona? Lazima itoke ndani, ambayo ni neno tangu mwanzo. [ 5 ]

Lakini unapokuwa umezaliwa na Roho wa Mungu, hapo sasa u mwana wa Mungu, na siku zote ulikuwa mwana wa Mungu, na siku zote utakuwa mwana wa Mungu. (Wagal. 4:6). Hakuna njia ya kulitenganisha hilo, kwa sababu unao uzima wa milele. Na uzima wa milele kamwe haukuwa na mwanzo; na wala hauwezi kuwa na mwisho. [ 6 ]

Kama u mwana wa Mungu, na kama mimi ni mwana wa Mungu au binti wa Mungu, tulikuwa ndani ya Mungu tangu mwanzoni. Na Yesu alipokuwa ukamilifu wa Neno, hapo sasa tulikuwa ndani Yake, katika namna ya chembe ndogo. Pale aliposulubiwa, tulisulubiwa katika mwili wake.
Alipofufuka kutoka kwa wafu, tuliinuka naye. Na sasa kwa vile tumelitambua hilo, sasa tumeketi pamoja na yeye mbinguni (Katika ulimwengu wa Roho) ndani ya Kristo Yesu (Waef. 2:6 – 7 ). Sisi kama ni wana na binti za Mungu; sisi ni watoto wa Mungu hivyo tu sifa za Mungu. Hapo sasa tunao uzima wa milele, na Mungu ni uzima wa milele pekee uliopo. Kwa hiyo tulikuwa ndani yake tangu mwanzo. Na Yesu alipokuwa lile Neno lote tulikuwa sehemu Yake hapo. Amen. Tunasimamia hapo. Hilo linapokuwepo pale, hakuna Shetani, hakuna nguvu, wala chochote kiwezacho kusogeza hilo. Hiyo ni nguzo ya nafsi inapofungiwa.

Unaweza ukapakwa mafuta hapa katika roho, na shauku, na kufanya haya yote, lakini inapokuja kwenye nguzo hii ya kufungia kwa lile Neno, kamwe huwezi kusogea pale. Itashikilia hasa bila kuyumba na kuwa kweli kwa lile Neno kadiri iwezavyo kuwa. Nje ya hilo, haijalishi unafanya nini bado umepotea.

Ule wakati wa Kanisa wa Laodikia, Uchi, kipofu, mwenye mashaka, na wala haujui hilo (Ufunuo 3:15 – 17). Unaona, haukupakwa mafuta, kupakwa mafuta na Roho halisi. Unaona kuwa Roho Mtakatifu anaweza akamshukia mtu katika roho yake, Lakini nafsi yake ndiyo mbegu. Hiyo mbegu ni Neno. Sijali unahubiri kiasi gani.



Unafanya hili vizuri kiasi gani, na jinsi unavyopenda sana …… Hiyo ni moja tu ya milango ya roho, huwezi ukapenda kwa mwili wako; unapenda kwa roho yako. Hiyo ni moja ya milango ya kuingilia. Na unaweza kupenda na hata kumpenda Mungu, na bado usiwe huko sahihi. Unaweza ukatoa pepo, na kuhubiri, na kufanya haya mengineyo, na bado usiwe sahihi. Yesu alisema hivyo; alisema wengi watakuja katika siku ile (Matayo 7:21 – 23 ). Hilo Neno linamaliza hilo. [ 7 ]

Kama wewe ni Mkristo sasa, mbegu halisi iliyokusudiwa (Luka 8:11, Matayo 13:37 – 38 ), ulikuwa ndani ya Mungu kabla hakujawa na ………. Siku zote ulikuwa ndani ya Mungu. Mbegu ya uhai wako, ambayo ni sifa za Mungu, ambayo ilikuwa mawazo yake ……..

Na ili mradi ni mbegu ndani inakuwa, lazima utazaa hasa ile mbegu ilivyosema inazaa (Mwanzo 1:12). Hiyo ni sawa kabisa. Ni Neno lake. Anashika Neno lake na kuliangalia hilo.

Na kama hukuwa ndani ya Mungu ………… kama unaamini ujumbe wa Biblia, na ujumbe wa saa hii, uthibitisho wa hiyo……… Sababu umeketi hapa, kwa sababu ulikusudiwa uketi hapa. Usingekuwa hapa kama sivyo; ungekuwa kule mitaani, labda umelewa, wengine wenu, na wengine; na wengine wenu nje kule wakitembea na wake za wanaume wengine; na ninyi wanawake nje mmeolewa, na mnatembea na waume wa wanawake wengine, au kitu kama hicho. Unaona" lakini ulikusudiwa kimbele uwe hapa (Rumi 8:29 – 30 ). Huwezi kujisaidia. Unaye Baba; Yeye ni Mungu, na wewe ulikuwa Mbegu.

Ulikuwa ndani yake pale kama wazo; sasa ni mtu ambaye mnaweza kuwa na ushirika naye. Unaona: Kama ulivyokuwa ndani ya Baba pale mwanzoni lakini sasa ni wana na binti, hivyo unaweza kuwa na ushirika na wazazi.
Sasa, tu wana na binti za Mungu, wanaoweza kuwa na ushirika na Baba, Mungu. Unaona, ni nzuri yakupendaza. Hulipendi hilo? Hivyo kuweni kama Yeye. Na kama tulikuwa wana, hapo sasa ni sifa, na tulikuwa katika umbile lake hapo mwanzo.

Chochote Kristo alicho, ndicho nilicho. Yeye alivyo, ndivyo nilivyo. Mungu. Kama aliwaziwa kuwa na akili, nami nitakuwa hivyo, Kama alikuwa beelzebub kwa kazi za Roho wake, ndivyo pia nilivyo. Vyovyote alivyokuwa, ndivyo nilivyo. Vyovyote alivyo, ndivyo ulivyo..

Sasa, anaweza kuwa na ushirika nasi au kupitia sisi, na kutulia katika Neno lake pamoja nasi. Ambavyo tu sehemu yake, Basi tu sehemu ya Neno. Na nawezaje kukanusha kuwa nina mkono? Haijalishi sayansi itasemaje kwamba sina mkono, mimi ninao mkono. Ninajua ninao mkono. Ninautumia.

Na ninajua ninaye Mungu. Ninaye Mwokozi. Namsikia ndani ya Nafsi yangu. Mimi ni sehemu yake. Vile tu hili Neno linavyosema; hivyo ndivyo nilivyo. Na kama naweza tu kukataa sehemu ya hili, hiyo ni sawa na kukataa kwamba ninao

mkono, sikio, jicho.  Siwezi kufanya hivyo na nibakie mwanadamu aliye kwenye akili zake timamu, wala siwezi kukana sehemu ya neno la Mungu na nibakie katika Roho sahihi ya Mungu.  Ni lazima nichukue kile ambacho madhehebu yanasema au kile Mungu anasema juu ya hilo.  Unaona?  Huwezi kufanya hivyo.   [ 8 ]

Kama unao uzima wa milele (Yohana 5:24 ), ulikuwa ndani ya Mungu kabla dunia haijakuweko wewe ni sehemu, mwana wa Mungu, sifa za Mungu.  Alijua hata wakati ambao wewe ungekuja.  Alikukusudia wewe kwa wakati huo kuchukua nafasi, na hakuna hata mmoja awezaye kuichukua.  Sijalishi kuna waigizaji wangapi na mambo, lazima uwepo pale, kwa sababu alijua utakuwepo pale.  Sasa , unadhihirishwa; Sasa unaweza ukawa na ushirika naye, na hivyo ndivyo anavyotaka. Anashauku na ushirika, kuabudiwa.  Lakini kama maisha yako siku zote hayakuwa ni sifa za Mungu, wewe ni mwigizaji tu wa Ukristo.  Unaona?  Watakuwepo Mamilioni na Mabilioni ya wao watakao kuwa waigizaji tu wa ukristo.  [ 9 ]

Sasa njia pekee uwezayo kuwa mwana au binti wa Mungu ……  kwa sababu uwe na uzima wa milele ….. Na kuna aina moja tu ya uzima wa milele, na huo ni uzima wa milele wa Mungu.  Uzima wa milele aina moja tu, ambao ulikuwa ni Mungu.  Ili uwe mwana wa Mungu, inakupasa uwe ulikuwa ndani yake siku zote.  Ile chembe ya uhai wako, uzima wa kiroho usiku wa leo, ulikuwa ndani ya Mungu baba kabla hakujawa na kitu.  Unaona?  Na wewe sio chochote ni udhihirisho tu wa chembe ya uzima ambao ulikuwa ndani ya Mungu kama mwana wa Mungu.  Sasa, unadhihirishwa, baada ya Neno lake kuja ndani yako ili kuangaza huu wakati.

Unaudhihirisha uhai wa Mungu ndani yako, kwa sababu u mwana au u binti wa Mungu.  Unalipata ninalo maanisha?  Umekaa katika kanisa hili usiku wa leo, kwa sababu wajibu wako ni kumdhihirisha Mungu kwa Taifa hili, na watu hawa, na watu hawa majirani unaojihusisha nao.  Popote pale ulipo, Mungu alijua kwamba utakuwa hapo, kwa sababu ni lazima uwe moja ya chembe chembe zake au sifa zake.  Lazima uwe hivyo.  Kama unao uzima wa milele, hapo sasa ilikuwa ni uzima wa milele siku zote.  Na Mungu kabla hakujawa na dunia alijua kuwa utakuwa hapa.  Na wakati wa kuoshwa na maji ya neno uliposhukia juu yako, ulidhihirishwa ndani ya kiumbe. Sasa, Unao ushirika na Baba yako, Mungu, kama vile tu ulivyo nao na baba yako wa duniani.  Unaona?  Ninyi ni wenyeji wa ufalme, sio wenyeji, lakini ni wana wa kiume na wa kike wa Mungu aliye hai kama ule uzima wa milele unakaa ndani yenu (Warumi 8:16 – 17 ).

Sasa, kama ilivyokuwa, Yesu alikuwa ukamilifu wa Mungu ukidhihirishwa.  Yeye alikuwa ukamilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili (Kolosai 2:9 – 10 ); kwa hiyo, alipokuja hapa duniani na akadhihirishwa katika mwili, ulikuwa hapa ukiwa ndani yake, kwa sababu alikuwa ni Neno.

“Hapo mwanzo kulikuwako Neno ………  Neno lilikuwa kwa Mungu na Neno lilikuwa Mungu.  Na Neno lilifanyika mwili na kukaa kati yetu …..” (Yohana 1:1 – 5, 14 – 18 ).



Neno lilifanyika mwili:  kwa hiyo, ulitembea Naye, alipo…………………ulikuwa ndani yake alipokuwa hapa duniani.  Uliteseka pamoja Naye, na ulikufa pamoja Naye; ulizikwa pamoja naye, na sasa umeinuliwa/umefufushwa pamoja Naye na udhihirisho wa sifa za Mungu, ukiwa umekaa katika ulimwengu wa Roho mbinguni, ukiwa umefufushwa tayari, umefufushwa kwa maisha mapya na kukaa katika ulimwengu wa kiroho ndani ya Kristo  Yesu. Oh, hilo linamaanisha sana katika siku hizi, kanisa.  Hilo linamaanisha sana kwetu sisi kuona nafasi zetu wenyewe tukiwekwa ndani ya Yesu Kristo   [10]

Unaona sasa, kama ulikuwa katika ufahamu wa mbele wa Mungu, sasa unakuwa sehemu ya Mungu na njia pekee uwezayo kuwa mwana wa Mungu au binti wa Mungu, ni kuwa sehemu ya Mungu, na Mungu hakukamilika bila ya wewe lazima iwe hivyo.  Hiyo ni sawa, kwa sababu kuna mmoja, mmoja tu chimbuko la uzima wa milele, na hilo ni Mungu, na yeye pekee anao uzima wa milele.  Unaona?  Sasa na wewe ulikuwa sehemu yake, kiasi kwamba wewe ni sifa zake, au katika mawazo yake kule mwanzoni.  Na kwamba, kwa sababu amekufikiri wewe tangu mwanzo, inaleta ule msukumo wa kumuelekea YeYe.  Hicho ndicho kitakiwacho huhuishwa. Wengineo hawawezi kuhuishwa; hawana hicho kitu cha kuhuishwa ndivyo hivyo tu. Ni kama tu ungeweka punje ya mhindi udongoni……………haijalishi ni nzuri namna gani, kama haina chembe ya uhai ndani yake, haiwezi kamwe kuhuishwa. Lakini ile punje ya uhai inabidi iwe pale kwanza.  [ 11 ]

Musa alikuwa ndani Yake.  Joshua alikuwa ndani Yake na kama uko ndani Yake, ulikuwa ndani Yake kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ile familia ya Mungu; uliteswa pamoja naye; ulikufa pamoja naye; ulienda msalabani pamoja Naye (Rumi 6:6); ulifufuka pamoja Naye; na sasa bado uko Naye, ukiwa umeketi katika ulimwengu wa roho, ukiangaza ujumbe wa wakati kwa dunia, ile nuru ya ulimwengu.  “Wewe ni Nuru ya ulimwengu” (Matayo 5:14-16) kwa sababu uko ndani ya Yesu Neno, sehemu ya Neno ambayo inadhihirishwa siku ya leo, ujumbe wa siku ya leo, sio Luther, Wesley, Pentekoste; lakini Yesu wako, anayeangaza ambaye amekuja katika hili huwezi uende nyuma katika lile; huko ni kuongeza chachu katika mkate wako Mtakatifu, ambao “Mtu haishi kwa mkate tu  bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu katika wakati wake”  (Matayo 4:3) [12]

Sasa, nasi sote hebu tuangalie shauku zetu, na hapo unaweza ukaona ni chujio la namna gani ambalo unachujia kupitia hilo.  Hebu tuangalie, kila mmoja wetu, hapa na kule  katika taifa lote.  Angalia shauku zako, unataka nini hasa katika maisha angalia unachopigania.  Angalia uko hapa kwa ajili gani.  Angalia ni kitu gani kinakufanya uende Kanisani ni kitu gani kinakufanya………….. Nivizuri kwenda kanisani, lakini usiende tu Kanisani; hilo halitakuokoa unaona?  Hebu jichunguze kwa dakika chache, sema kusudi langu ni ……………Ninachujia kupitia chujio la aina gani hata hivyo?” Na kama huwezi kukubaliana na Neno la Mungu, na nafsi yako haifanyi hivyo, sasa kuna kitu siyo sahihi, kwa maana inaonyesha ladha yako, ni uhai wa aina gani uko ndani yako kama ni mtakatifu, wa uaminifu, wakuheshimiwa, utakuja kuonekana hivyo kama sivyo unayo ladha ya aina nyingine

ambayo unachujia, hivyo ni sawa kabisa. Na kama radha ni Neno la Mungu na mapenzi ya Mungu, hapo sasa unajua kilichoko ndani yako, kile kinachovuta radha inaonyesha u sehemu ya lile Neno. Lile Neno liko ndani yako likichukua likivuta kutoka kwenye Neno. Linavuta nini? Linachukua kupitia lile neno kwa sababu u sehemu ya mwili wa Kristo wa wakati huu. Na kama lile Neno liko ndani yako, itachukua tu kutoka katika Neno yule Roho ambaye analihuisha lile Neno ambalo liko ndani yako (Yohana 6:63; 2 kor 3:6). Lile Neno peke yake haliwezi kuishi. Hiyo ndiyo sababu, "Wote alionipa Baba watakuja kwangu (Yohana 6:37), na kama nikiinuliwa, nitawavuta wote waje kwangu" Unaona, unaona? Baba……………………

Sehemu ya mwili wa Kristo iliyoko duniani, ilikusudiwa kimbele, ikawekwa ndani ya moyo……………..mtu yoyote aliye mkristo halisi, akiwa amezaliwa mara ya pili leo, anafahamu tangu alipokuwa mtoto mdogo au msichana mdogo yeyote, kwamba kulikuwa na kitu ndani yako kilichokuwa kinamuonea Mungu shauku (njaa) Matayo 5:6) Na ulijaribu kujiunga na makanisa na kila kitu kingine; haingesaidia ilikuwa ni nini? Ilikuwa ni Neno. Ulikuwa unawinda upate chujio, na siku moja ikawaka mbele zako; ukamuona Yesu Kristo yule yule jana na hata milele (Waebr 13:8). Hilo lilitosheleza ile shauku unaona? Kwa sababu uzima ulikuwa ndani yako ukivuta unaona uhai ulioko ndani yako unavuta; umewekwa kwa shauku uliyonayo hapa unavuta…………..Huwezi ukavuta kupitia hiki au kile kinginecho; lazima utafute lile chujio sahihi (chujio la Mungu, Neno la Mungu), kwa sababu ni mtu anayefikiri.

Lile Neno, kama umechaguliwa kimbele, unaliona hilo. Hakuna njia ya kulificha kwako. Unaangalia pale na kusema, hilo hapo. Ninaliangalia moja kwa moja. Ninaliona. Hili hapa lile Neno, kila Neno, neno kwa neno, linaishi" Hapa sasa kuna kuna kuuonja uzima wa milele ambao unauhitaji. Na unapopumua kupitia huo………………ni kitu gani kiwezacho kupitia hapo? Kwenye chujio la Mungu? Hakuna ila Roho, hakuna dunia hata, hakuna kutokuamini hata. Ni chujio la Mungu na unapo pumua kupitia hilo, hakuna kiwezacho kupitia hapo ila Roho Mtakatifu.

Sasa, unao ushahidi wa Roho Mtakatifu unaona? Mtu mtakatifu au radha ya mwanamke anayependa kuishi, anao uzima wa milele. Na kwa sababu hili Neno halijahuishwa kwao, wanaishi.

Nami najua, ikiwa sisi tu sehemu yake au siyo, Ninaamini kwamba tu……………..lakini kama siyo, kuna mtu fulani duniani leo ambaye ni sehemu ya mwili wa Kristo; na utaishi tu kwa Neno la Mungu, kila Neno ambalo limetoka kwa kinywa cha Mungu kwa wakati huu ambao tunaishi sasa.

Angalia lile Neno haliwezi kujikana lenyewe. Kwa hiyo ni ile shauku. Ni shauku? Kwa sababu ndani katika nafsi yako kulikuwako mbegu iliyokusudiwa kabisa uzima wa milele siku zote ikiwa imekaa pale……………………… siku zote ilikuwapo pale" wote alionipa Baba watakuja kwangu (Yoh 6:37 – 39, 44). Hakuna hata mmoja atakayepotea"



"Ladha ya mtu anayefikiri….." Wakati mtu anayefikiri anasikia Neno la Mungu, "Kondoo wangu wanaisikia sauti yangu, mgeni hawatamfuata" (Yohana 10:27 – 29), kwa maana chini pale kuna uhai/uzima na uhai unaunganika na uhai/uzima. Dhambi inaunganika na dhambi, na dhambi ni ya kinafiki sana mpaka inafikiri kwamba imeokotwa wakati haikuokotwa. Iko katika kilima (kilindi) cha unafiki. [ 13 ]

Katika mawazo ya Mungu; Mungu, yule Roho mkuu. Hapo mwanzo, kabla haujawepo mwanzo, Alikuwa Mungu, na je ulijua ulikuwa ndani Yake wakati huo? Kama wewe ni Mkristo sasa, ulikuwa ndani Yake wakati huo.

Na sasa, kama ni hivyo, ule utumilifu wote wa uungu uliumbwa katika utu wa Yesu Kristo. Na halafu Yesu alipo kufa pale msalabani pamoja Naye. Tulienda kaburini pamoja Naye. Na tulifufushwa pamoja naye katika ufufuko na sasa tumepaa, kwa roho wake, mpaka kwenye kiti cha rehema, tukiwa tumekaa katika ulimwengu wa kiroho ndani ya Yesu Kristo siku zote! [ 14 ]

**Nukuu za kiingereza**


(1) "Ibrahim" (56 – 1208), Aya 20
(2) Njia Mungu aliyotuwekea kwa ushirika (60-0709), Aya 26
(3) "Mkutano" (63-0608), Aya 43-44
(4) Muungano wa siri wa Bibi Arusi uk 10
(5) "Nawe hujui" uk 28
(6) "chujio la mtu anayefikiri", Aya 71
(7) Kristo akifunuliwa katika Neno lake mwenyewe Aya 28-30
(8) "Nguvu ya kubadilisha" (65-103M), Aya 291 – 304
(9) "Kunyakuliwa" Aya 85
(10) "Mambo yatakavyokuwa" Aya 32-32a
(11) "Usizitegemee akili zako mwenyewe" Aya 17
(12) "Mahali pekee Mungu alipopachagua pakuabudia" (65-1128) Aya 271/278
(13) "Chujio la mtu anayefikiri" Aya 163 – 164, 180 – 184, 108 – 109
(14) "Mungu wa wakati huu muovu" Aya 67



*jiwe la kiroho la kujengea na 163 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fas : (+49) 72353306.*


*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.*

*(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*


*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa:*


*Charles E. Y. Kenju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.co*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*